

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA ISHIRINI**

**30 APRILI, 2026**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA TATU

**KIKAO CHA ISHIRINI – TAREHE 30 APRILI, 2026**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

### **III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

### **IV. MASWALI YA KAWAIDA:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):**

#### **233. MHESHIMIWA STELLA ALEX IKUPA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali imefikia wapi katika utekelezaji wa Waraka wa TAMISEMI wa 10/7/2017 kuhusu kutenga maeneo ya Biashara kwa Watu wenye Ulemavu.

#### **234. MHESHIMIWA EDIFONSI JOACKIM KANONI (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Daraja la Mto Saise litakalo unganisha Kata ya Mambwe Nkoswe na Mambwe Kenya.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**235. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu ya upandaji miti ili Wananchi washiriki kikamilifu katika biashara ya *Carbon* hasa wale wa Vijijini.

**WIZARA YA UJENZI:**

**236. MHESHIMIWA DKT. EMANUEL QAMBAJI NUWAS (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali inampango gani wa kuanza ujenzi wa Barabara ya lami kutoka Haydom hadi Labay.

**237. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha Changarawe Barabara ya Kipengele - Lupila ambayo inaunganisha Halmashauri ya Wanging'ombe na Wilaya ya Makete.

## **WIZARA YA UCHUKUZI:**

### **238. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga Gati ya Kontena katika Bandari ya Tanga.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **239. MHESHIMIWA MOHAMED MUSSA UTALY (LINDI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga upya nyumba za Askari Polisi Lindi Mjini ili kuboresha mazingira ya makazi na kuongeza ufanisi kwenye ulinzi na usalama.

## **WIZARA YA NISHATI:**

### **240. MHESHIMIWA BAZILIO KAPUNDA MBWILO (NKASI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, nini matokeo ya utafiti wa Mafuta na Gesi katika Ziwa Tanganyika upande wa Jimbo la Nkasi Kaskazini.

## **WIZARA YA MADINI:**

### **241. MHESHIMIWA MABULA JOHNSON MAGANGILA (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, lini Serikali itatenga maeneo maalum ya Wachimbaji wadogo katika Halmashauri ya Msalala.

## **WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

### **242. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Minara ya simu katika Hifadhi ya Mkomazi.

## **V. HOJA ZA SERIKALI:**

### **WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**DODOMA  
30 APRILI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD  
KATIBU WA BUNGE**